**HALMASHAURI YA WILAYA RORYA**

SHULE YA SEKONDARI KIROGO

**SIMU:** 0787409141 S.L.P 88

0767409144 TARIME

TAREHE …………………

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIROGO KIDATO CHA KWANZA MWAKA WA MASOMO 2024**

## 1.0 TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI

Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo unaoanza Januari 2024.

Aidha nachukua nafasi hii pia kumpongeza mwanao kwa kupata nafasi hii muhimu ya kuendelea na masomo ya sekondari na nina hakika ataitumia ipasavyo ili kujenga maisha yake ya baadaye na Taifa kwa ujumla.

Shule ya sekondari KIROGO Iko magharibi umbali wa km 30 toka makao makuu ya Hamashauri ya wilaya RORYA.

Shule hii ni ya kutwa lakini **huduma ya chakula cha Mchana inapatikana shuleni** kwa utaratibu wa wazazi wa wanafunzi kuchangia kadri ya makubaliano ya mikutano ya wazazi na Bodi ya shule.

**Muhula wa masomo** unaanza rasmi **TAREHE 08, JANUARI, 2024** Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo bila kukosa ili asipitwe na masomo ikiwa ni pamoja na kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza endapo hataripoti mapema hususani baada ya wiki mbilo za mapokezi ya kidato cha I.

### 1.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

A) WASICHANA

i) Sketi **mbili**(2) moja damu ya Mzee yenye michirizi 2 myeupe katikati na nyingine rangi ya nyeusi( iwe na michirizi 2 myeupe katikati), zote ziwe

ndefu hadi chini kitambaa cha suti, zenye kufunika vifundo vya miguu, rinda box(6 mbele na 6 nyuma), pindo liwe inchi 1. (Wasichana)

ii) Shati **mbili**(2)nyeupe zenye mikono mifupi( TOMATO SHIRT) kwa wote.(Wavulana na wasichana)

iii) Viatu vyeusi pea **mbili(2)** vya ngozi vyenye kufungwa na gidamu( kamba), vyenye visigino vifupi na visiwe buti kwa wote. (Wavulana na Wasichana)

iv) Soksi nyeupe ndefu pea 2 na zaidi.

B)WAVULANA

v) Suruali **mbili(2)** moja rangi ya **damu ya Mzee** na nyingine rangi nyeusi, zote zishonwe kwa kutumia kitambaa cha suti na ziwe na turn up ya sentimita 16. Kamwe suruali aina ya modo hazitakiwi kabisa shuleni wakati wote na zitachomwa kwa moto. (Wavulana)

vi) Soksi nyeusi ndefu jozi mbili(2) au zaidi kwa Wavulana

vii) Viatu vya michezo jozi moja (**raba nyeus**i) kwa wanafunzi wote.(Wavulana na wasichana)

viii) Mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana tu. (Wavulana lazima wavae suruali kwa mkanda)

ix) Sweta moja rangi ya damu ya Mzee kwa wote. (Wavulana na wasichana)

x) *T-shirt moja rangi ya zambarau yenye kola (Wavulana na wasichana).*

xi) Jozi moja ya nguo za michezo (**Trucksuit**) rangi ya bluu bahari yenye michirizi myeupe. Uoneshwe rangi shuleni.(pia zinapatikana shuleni gharama tsh 25000)

***xii)*** Hijab rangi **nyeupe** zisizokuwa na urembo kwa wanafunzi waislamu(wasichana) ivaliwe kwa suruali pana na nusu kanzu rangi damu ya Mzee na nyeusi kulingana na ratiba ya sare ya shule siku husika

xiii) T-shirt ya michezo rangi ya blue( mikono mifupi).

.

NB***: Hakikisha suruali yako mkanda unafunga kiunoni na siyo kwenye makalio***.

2.2 VIFAA VYA DARASANI

i) Daftari za kaunta (quire 4au 3) 12 ii) Mkebe (mathematical set) 01

iii)Kalamu za wino 10 ( iv).School bag 01 (V) ream 01 (kwa ajili ya kufanyia mazoezi na test pamoja na mitihani mbalimbali

( iV) Faili moja la kutunzia mitiani. Aina ya faili ni **File Folder** rangi ya kaki

V) **Dictionary ya kiingereza kwa kiingereza** ili mwanafunzi apate urahisi wa kujifunza lugha ya kiingereze

vi. Vitabu **viwili(2)**vya hadithi(**Hawa The Bus Driver** na **Mabala The Farmer)**

**Vii.** Ream paper moja(1)aina ya **double A k**wa ajili ya **mitihani na mazoezi** mbalimbali

Viii. TSH 10,000/- kwa ajili ya Taaluma .

**2.3 VIFAA VYA USAFI**

(i) Ndoo mpya **moja(1)** yenye ujazo Lita 10 au zaidi kwa wasichana

(ii) Jembe moja(1) lenye mpini.

**2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na ,Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. **Hivyo** Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yote ya msingi yafuatayo

i. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri na kuwahi katika kila shughuli ndani na nje ya shule na kuzingatia ratiba ya shule ni lazima.
iii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote.
iv. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
v. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.
vi. Kutunza mali ya shule.

## 0.4 MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi;
(ii) Utoro au Kutohudhuria masomo darasani / shuleni kwa muda mrefu bila taarifa
(iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo;
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii
(v) Kupiga au Kupigana, kumdharau mwalimu au mfanyakazi mwingine
(vi) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(vii) Uvutaji wa sigara;
(viii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa;
(ix) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xi) Kusababisha mimba au kumpa mimba mwanafunzi;
(xii) Kwenda kwenye majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni;
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa;
(xv) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
(xvi) Kukataa adhabu kwa makusudi

4.0 MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI.

a) Medical examination form, ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelezo mengine yatakayo tolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwamakini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***HAKIKISHA FORM ZOTE ZINAJAZWA VIZURI NA KWA USAHIHI ,USIPO JAZA HAUTAPOKELEWA.***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**………………………………**
**ELISHA J. ANDREW**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIROGO**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**.

**Jina kamili la mwanafunzi** …………………………………………………….............

Taifa …………………………………. Mkoa ………………………. Wilaya……………..

Tarehe ya kuzaliwa ………………………………….

Lugha unayozungumza nyumbani…………………….

Kabila …………………

Jina kamili la Baba……………………………………Amefariki/Hai **(kata isiyohusika)**

Jina kamili la Mama ……………………………………Amefariki/Hai **(kata isiyohusika)**

Jina kamili la mlezi( kama huna mzazi)

…………………………………………………………………………………………

Uhusiano na mlezi

…………………………………………………………………………………………

Kazi ya Baba ……………………………… kazi ya Mama ………………………………

Kazi ya Mlezi ………………………………

Je umewahi kuwa kiongozi katika shule ya msingi uliyotoka? NDIYO/HAPANA.Kama ndiyo kiongozi wa Nyanja ipi? (Taja) ……………………………………………………..

Michezo uipendayo :1 …………………… 2 ……………......... 3…………………….

Unamatatizo yoyote ya kiafya? NDIYO/HAPANA. Kama ndiyo taja

………………………………………………………………………………

**Mawasiliano ya sasa ya mzazi au mlezi wako**

Jina ………………………………………….
Anwani ……………………………………..
Namba za simu (Baba) ……………………….…. (Mama) ……………………………..

(Mlezi)…………………………….

Jina la mwanafunzi ………………………………………… Saini .........................
Tarehe ……………….........

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIROGO**

**a) Mwanafunzi**

Nimesoma na kuzielewa sheria, Kanuni na taratibu zote za shule na ninakubali/sikubali kujiunga kusoma katika shule hii.

Ninaahidi nitazifuata sheria zote na kuzitekeleza kwa mujibu inavyotaka. Na endapo sitafuata taratibu na sheria hizo basi nirudishwe nyumbani kwa wazazi/walezi wangu.

Jina …………………………………… saini ………………….. Tarehe ………………..

**b) Mzazi/mlezi**

Nimesoma sheria, taratibu na kanuni za shule na kuzielewa. Nimekaa na mtoto wangu na tumekubaliana kufuata na kuzingatia sheria,kanuni na taratibu zote, hivyo hatavunja sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Nimekubali kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na shule. Kijana wangu hana simu ya mkononi na sitampa simu kwa matumizi yoyote .

i.

Jina ………………………………………….. saini …………………………

Simu ………………………………………. Tarehe ………………………

NB: ***Tafadhali soma maagizo/maelekezo na kuyatekeleza kikamilifu***

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**RORYA DISTRICT COUNCIL**

**KIROGO** SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 88

**TARIME**

DATE ……………………….

**PHONE NO. 0787409141.**

**Ref. NO.**KIR/SS/1/ …….

**To Medical Officer**

……………………………….

……………………………….

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please, Examine ……………………………………………………….. as to his or her fitness for pursuing secondary studies in this school.

**General condition of his or her health**:

Eye/vision ………………………………… Urine …………………………………

Ears/hearing ……………………………….. Pregnancy ……………………………

Mouth/speech ……………………………… Leucocytes …………………………

Nose ……………………………………… E.S.R ………………………………..

Blood group ………………………………… HB ………………………………….

Stool …………………………………………

Others ………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE / RECOMMENDATION**

I have examined the above named student, I consider and recommend him or her is **Fit / Not** fit for studies.

Special medical recommendation (**if any**)

………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**Signature of medical officer**. ………………………..

**Official stamp.**

………………………………………..